TANGAZO LA SERIKALI Na. 488 la tarehe 14/6/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*( Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MASOKO, MAGULIO NA MINADA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko, Magulio na Minada ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chumba" maana yake ni chumba au jengo lolote linalotumika kuuzia bidhaa ndani au nje ya soko pasipo kuhusisha meza, kizimba au nafasi wazi;

"chombo cha moto" maana yeke ni gari la abiria au gari la mizigo, na inajumuisha na lori, basi, bajaji na pikipiki;

"gulio" maana yake ni eneo maalumu au sehemu yoyote ya wazi iliyotengwa na Halmashauri au serikali ya kijiji kwa ajili ya shughuli za kuuza au kununua mazao ya nafaka, misitu, uvuvi au mifugo au bidhaa za viwandani kwa siku maalumu;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa;

"mfanyabiashara" maana yake ni mtu binafsi, taasisi, kampuni au kikundi cha watu wanaojishuhulisha na shughuli za kuuza na kununua bidhaa au mazao kwa lengo la kupata faida;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa pamoja na afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnada" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa na kumilikiwa na Halmashauri au serikali ya kijiji kwa ajili ya wafanyabiashara kununua au kuuza mazao au mifugo au bidhaa za viwandani;

"mnunuzi" maana yake ni mtu au kikundi cha watu, kampuni au shirika lolote linalonunua bidhaa au mazao au mifugo katika eneo la mamlaka ya Halmashauri;

"muuzaji" maana yake ni mtu yeyote anayeuza bidhaa au mazao au mifugo katika eneo lililoidhinishwa na Halmashauri;

"soko" maana yake ni eneo lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kutolea huduma na biashara za mazao na bidhaa mbalimbali;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri;

Wajibu wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kuanzisha, kusimamia na kuendesha masoko kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) kuendeleza masoko, magulio na minada;
(c) kusimamia usafi na usalama wa masoko, magulio na minada;
(d) kusimamia ufikishaji wa huduma za kijamii katika masoko, magulio na minada;
(e) kugawa na kupangisha soko kwa vyumba, meza au vizimba;
(f) kutenga maeneo kwa ajili ya magulio na minada; na
(g) kusajili wafanyabiashara wote katika masoko

yote ya Halmashauri.

Wajibu wa Afisa Mwidhiniwa

5. -(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha usalama unadumishwa kwenye eneo la gulio, soko au mnada kwa kuweka utaratibu mzuri wa ulinzi wa askari mgambo.

(2) Afisa Mwidhiniwa ataingia kwenye maeneo ya gulio, soko au mnada kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha kuwa Sheria Ndogo hii inazingatiwa.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

6. Mtu anayeingia katika gulio, soko au mnada kwa lengo la kufanya biashara au anayeingiza chombo cha moto katika gulio, soko au mnada atalipa ada au ushuru kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Muda wa kufanya biashara

7. -(1) Magulio, masoko na minada yote yatafunguliwa saa kumi na mbili asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili na nusu jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mtu hataruhusiwa kufanya biashara katika gulio, soko au mnada kabla ya muda wa kufungua au baada ya muda wa kufunga.

Wajibu wa kufanya usafi gulioni, sokoni au mnadani

8. Kila mfanyabiashara katika gulio, soko au mnada atapaswa kuhakikisha kwamba-

(a) anaweka eneo lake la biashara katika hali ya usafi wakati wote;
(b) anahifadhi taka kwenye ndoo au chombo maalumu chenye mshikio na mfuniko; na
(c) anatupa taka kwenye eneo lililotengwa na Halmashauri.

Uteuzi wa Wakala

9. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua mtu binafsi, kikundi cha watu, taasisi, au kampuni iliyosajiliwa kuwa Wakala kwa madhumuni ya Sheria Ndogo hii, ambaye atakuwa na jukumu la-

(a) kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri;
(b) kutoa maelekezo na maagizo juu ya usafi,

hifadhi ya mazingira na namna bora ya kuendesha shughuli za gulio, soko au mnada kulingana na maagizo au maelekezo ya Halmashauri;

(c) kuendesha na kudhibiti gulio, soko au mnada kulingana na Sheria Ndogo hii pamoja na maagizo atakayopewa na Halmashauri.

Makosa

10. Mtu anatenda kosa ikiwa-

(a) anamshawishi mtu au kikundi cha watu wasilipe ushuru;
(b) anakataa au kukwepa kulipa ushuru;
(c) anamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake;
(d) anauza au kununua bidhaa nje ya eneo la gulio, soko au mnada;
(e) anauza au kununua bidhaa kabla ya muda wa kufungua au baada ya muda wa kufunga;
(f) anashindwa kuzingatia kanuni za usafi;
(g) anafanya biashara nyingine zaidi ya ile iliyoruhusiwa;
(h) anakataa au kukwepa kulipa ushuru; au
(i) anamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

11. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa T.S Na.175 la 2013

13. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Magulio, Masoko na Minada) za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa za Mwaka, 2013 zinafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6)*

SEHEMU YA KWANZA

VIWANGO VYA ADA YA KUUZA MIFUGO

| NA. | AINA YA MIFUGO | KIWANGO CHA ADA |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Tshs. 3,000/= kwa kila Ng'ombe aliyeuzwa |
| 2. | Nguruwe | Tshs. 2,500/= kwa kila Nguruwe aliyeuzwa |
| 3. | Punda | Tshs. 3,000/= kwa kila Punda aliyeuzwa |
| 4. | Mbuzi | Tshs. 2,000/=kwa kila Mbuzi aliyeuzwa |
| 5. | Kondoo | Tshs. 2,000/= kwa kila Kondoo aliyeuzwa |
| 6. | Kuku/ bata/kwale/kanga na jamii yote ya ndege | Tshs. 200/= kwa kila Mfugo uliouzwa |

SEHEMU YA PILI

ADA YA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA

| NA | AINA YA MNYAMA/MFUGO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2,500/= |
| 2. | Mbuzi/Kondoo | 1,500/= |
| 3. | Nguruwe | 1,500/= |
| 4. | Kuku | 500/= |

SEHEMU YA TATU

USHURU WA KUINGIZA CHOMBO CHA MOTO KATIKA ENEO LA GULIO, SOKO AU MNADA

| NA | CHOMBO CHA MOTO | KIASI CHA USHURU KWA SIKU |
|---|---|---|
| 1 | Tani 0-3 | Tshs. 1,000/= |
| 2 | Zaidi ya tani 3-10 | Tshs. 3,000/= |
| 3 | Zaidi ya tani 10 | Tshs. 5,000/= |

JEDWALI LA PILI

———

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12)*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Kondoa, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …........… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya ….............… ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko, Magulio na Minada ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU :

Jina:…………………………………..…………………….....

Saini……………………….…………………………..………

Wadhifa: …………………………………………………………

Tarehe……………………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa uliofanyika tarehe 28/4/2022 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

SHABANI KAPALA MILLAO,
*Mkurugenzi Mtendaji (w),*
*Halmashauri ya Wilaya Kondoa*

ABDALLAH SALUM MAGUO,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya Kondoa*

**NAKUBALI**,

L.S

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-Tamisemi*